

Mathayo 9 : 18 - 25

Viongozi wa dini walikuja kwa Yesu na wakasema “**Binti yangu sasa hivi ameshafariki, njoo uweke mkono wako juu yake nae ataishi.**” Akaondoka Yesu akafuatana na wanafunzi wake.

Wakati yupo njiani, akakutana na mwanamke mmoja, alikuwa na ugonjwa wa kutoka damu kwa muda wa miaka 12 na kugusa upindo wa kanzu ya Yesu,



kwa maana alisema moyoni mwake “**nikigusa tu upindo wa kanzu yake nitapona.**” Yesu akamwambia “jipe moyo binti yangu, **Imani** yako imekuponya,” yule mwanamke amepona toka saa ile.

Yesu alipofika nyumbani kwa yule mjumbe. Aliona wapiga filimbi wakifanya maombolezi, akawambia “ondokeni, huyu msichana hajafariki, bali amelala wakamcheka sana,” waombolezaji walipoondoka Yesu aliingia na kumshika yule msichana, na yule msichana alisimama

